**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**Anuaniyasimu "ELIMU"**
**Simu: 026 296 35 33**
**Baruapepe:info@moe.go.tz**
**Tovuti: www.moe.go.tz**
**Unapojibu tafadhali taja:**

Mji wa Serikali -
Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
**40479 DODOMA**

**Kumb.Na. CA. 229/238/01A/65**

**20 Februari, 2025**

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P.63088,
**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P.1454,
**DAR ES SALAAM.**

Katibu Mtendaji,
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE),
S.L.P.13346,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
Baraza la Sunnar Tanzania (BASUTA),
S.L.P.8581,
**DAR ES SALAAM.**

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S. L. P. 13547,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
TAWOSCO,
S. L. P. 2458,
**DODOMA.**

Umoja wa Wazazi Jumuiya ya CCM,
S.L.P. 3,
**DODOMA.**

## WARAKA WA ELIMU NA. 03 WA MWAKA 2025 KUHUSU MFUMO WA KITAIFA WA KUWEZESHA SHULE KUWA JUMUISHI ZAIDI

### 1.0 Maelezo ya Awali

Mfumo wa elimu jumuishi unahusu juhudi za makusudi za kuanzisha, kuendeleza na kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu kuwa salama, rafiki na wezeshi kwa kila mwanafunzi kutoka makundi yote ikiwemo wenye mahitaji maalumu. Mfumo huu unaweka kipaumbele katika kujenga jamii jumuishi na mazingira jumuishi ya kufundishia na kujifunzia ambayo huwasaidia wanafunzi wote, kwa kuzingatia uwezo wao, ulemavu au mitindo ya kujifunza. Inahusisha kuunda utamaduni wa utoaji elimu unaothamini utofauti na uthamani wa kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata fursa zenye uwiano sawa katika kujifunza.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 na Mitaala ya Elimu iliyoboreshwa imesisitiza kuwa, wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu wapewe fursa sawa katika kujifunza, kushiriki, na kukamilisha mzunguko wa elimu katika mazingira jumuishi ili wapate umahiri uliokusudiwa. Ili kufikia azma hiyo, Wizara imeandaa Waraka unaotoa maelekezo kwa watendaji na wadau wa elimu kuhamasisha na kutekeleza mfumo wa elimu jumuishi katika shule zote nchini. Dhana ya kuwezesha **shule kuwa jumuishi zaidi** inalenga kujenga uelewa wa viongozi, walimu na watumishi mwega katika shule kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wazazi/walezi na jamii katika shughuli za ujifunzaji na maendeleo ya wanafunzi kwa ujumla wanapokuwa shuleni na nyumbani. Kwa kusema hivyo, **ujumuishi fanisi ni ule unaolenga utoaji wa elimu bora kwa makundi yote ya wanafunzi wakiwa katika mazingira ya shule na nyumbani.**

## 2.0 Malengo ya Waraka

Waraka huu unalenga kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na mfumo jumuishi zaidi katika utoaji wa elimu na kwa kufanya hivyo, pamoja na mambo mengine, **kupunguza mdondoko wa wanafunzi** kwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule, familia na jamii kwa ujumla.

## 3.0 Hatua za Kuchukua

Kwa Waraka huu, Wizara inawakumbusha na kuwaagiza Wamiliki wote wa shule kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali kutekeleza yafuatayo:

a) kuhamasisha na kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi;
b) kubaini shule zenye viashiaria mahsusi vya changamoto za ujumuishi, na kutengeneza mipango maalumu ya kurekebisha mapungufu hayo katika ngazi ya shule, familia na jamii;
c) kuendesha mafunzo kwa watekelezaji wa Kiunzi cha Kuwezesha Shule kuwa Jumuishi Zaidi katika Ngazi Zote; na
d) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa uwezeshaji wa shule kuwa jumuishi.

## 4.0 Utekelezaji wa Waraka Huu

Waraka huu na Nyaraka zote zilizowahi kutolewa kabla ya Waraka huu na Ofisi ya Kamishna wa Elimu zitaendelea kutekelezwa isipokuwa pale ambapo maelekezo yaliyotolewa awali yanapokinzana na utekelezaji wa Waraka huu.

Waraka huu unaanza kutumika kuanzia tarehe **21 Februari, 2025**.

**5.0** Nawatakia utekelezaji fanisi.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** **Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule wa Wilaya**
**TANZANIA BARA**